



UWASILISHAJI WA MADA



UTEKELEZAJI WA MFUMO WA UNUNUZI WA UMMA KWA NJIA YA MTANDAO, UZOEFU KUTOKA KWA WAZABUNI.

**KAMA ILIVYOWASILISHWA NA MHANDISI
Matokeo Owden
Kwa niaba ya wakandarasi**





YALIYOMO



- ❖ Utangulizi
- ❖ Faida ya Mfumo
- ❖ Changamoto za Mfumo
- ❖ Mapendekezo/Maboresho/Ushauri





Muwasilishaji



- ❖ Engineer Matokeo Owden.
- ❖ Professional Mechanical Engineer.
- ❖ Md Tribute Tanzania Ltd.
- ❖ Katibu Mkuu Msaidizi, Arusha Allstars Veterans.
- ❖ Mechanical Contractor Class 3
- ❖ Tunahusika na Utengenezaji na Uuzaji wa Majenereta, Vipuli vya Magari, Mitambo ya Ujenzi, Air Conditions etc.
- ❖ Tupo Sakina Arusha -Opposite Arusha Meat.





Faida za Mfumo



- Hakuna Urasimu, hukutani na mtu yoyote. Ni wewe na mfumo wako. Hivyo Hakuna Mianya yoyote ya Rushwa.
- Mfumo huu unaokoa muda na fedha
- Mfumo huu unahifadhiwa katika mfumo wa Tarakilishi (computer) na hivyo ni rahisi kutunza kumbukumbu na kuzitumia ukizihitaji.
- Mfumo unatoa taarifa mbalimbali za Zabuni na za ufafanuzi kwa wadau kila wakati





Faida za Mfumo



- Kama hujakidhi vigezo vya viambatanisho mfumo huu unakukataa na hivyo huwezi kulalamikia kukosa tuzo.
- Mzabuni anapata fursa ya kushiriki zabuni ndogo ndogo.
- Inaondoa mizunguko ya kutafuta zabuni zisizo za lazima.
- Mfumo huu umerahisisha wepesi wa kurudisha zabuni.





Faida za Mfumo



- Inaonesha Orodha yote ya zabuni zote zilizoombwa na mzabuni husika.
- Inaonesha tuzo zote za zabuni zilizotolewa kwa wazabuni
- Unaweza kuona taasisi zote zinazotangaza zabuni ili mradi wamejiunga kwenye mfumo





Faida za Mfumo



- Muomba zabuni anapata fursa ya kushiriki kikamilifu kwenye zabuni; hii ikiwa ni pamoja na kuomba ufafanuzi wa jambo lolote kupitia mtandao na ufafanuzi huo na majibu yake yanakuwa wazi kila mdau, hivyo inaleta uelewa wa pamoja



Faida za Mfumo



- Gharama za zabuni kwa mfumo huu ni ndogo sana, elfu 30 tu na pia hazibadiliki badiliki.
- Muomba zabuni hawezi kupoteza zabuni zake
- Wakati wa kujaza zabuni ni nyaraka chache sana zinazohitajika na utazona kwenye viambatanisho vinavyohitajika au utazona wakati unaanza kuambatanisha kwa ajili ya kutuma zabuni.





Faida za Mfumo



- Umekuza usawa na kupunguza malalamiko mengi ya kutoa zabuni kwa upendeleo.
- Mzabuni anayeshinda sio siri, jina lake linawekwa wazi na bei zinakuwa wazi.
- Gharama za nakala na za Kuchapisha zimeondolewa na mfumo huu kwasababu kila kitu kinaambatanishwa kwa Tarakilishi





Changamoto za mfumo



- ❖ Nakala na viambatanisho vyote vinatakiwa kuwa katika nakala laini (soft copy).
- Mtumiaji lazima awe anajua vizuri matumizi ya Tarakilishi (Computer).
- Matumizi ya mfumo huu unategemeana na uwepo wa mtandao husika
- Kwasababu kila kitu kinategemea mtandao, mara nyingi Huduma hii haitaki uharaka; inataka uanze mapema hatua kwa hatua kabla ya siku ya mwisho wa kurudisha zabuni.



Changamoto za mfumo



- Mzabuni anayepata tuzo ukiondoa vigezo vingine kigezo kikubwa ni bei ya chini, jambo ili linaweza kuathiri ubora na ufanisi wa muda kwa aliyepata tuzo.
- Kwasababu ya **kigezo cha lowest evaluated bidder**; Wakandarasi wakubwa wenye viwango wamekuwa wakiacha kuomba baadhi ya kazi.
- Kwasababu hiyo hiyo baadhi ya wazabuni wameacha kuomba zabuni





Changamoto za mfumo



- ❖ Baada ya ufunguzi wa zabuni, Wakati mwingine inakuwa ngumu sana kupata matokeo ya zabuni uliyoomba kwasababu unakuta pengine zabuni 1000 zimetolewa na hazijapangwa kwa alphabeti hivyo inakuwa ngumu kuona majibu ya zabuni yako.





Changamoto za mfumo



❖ Wakati wa urudishaji wa zabuni kuna hatua mbalimbali za kufuatwa, wakati mwingine ukijisahau kusevu nyaraka ambatanishi kuna wakati ukiwa unazituma inakuambia hakuna kiambatanisho ulicho ambatanisha hivyo yakubidi kuanza upya.





Ushauri na Maboresho



- Wakati wa kufanya marekebisho ya mfumo kuwe na taarifa za mapema kwa wadau au watumiaji wa mfumo.
- Kuwe na Utaratibu maalumu kimikoa au kikanda wa mafunzo kwa watumiaji mara kwa mara kama mlivyofanya sasa.
- Kigezo cha Lowest Evaluated Bidder kiangaliwe upya.
- ❖ Kuwe na Ofisi japo ya kanda kwa kila kanda.





Ushauri na Maboresho



Pia vigezo vinavyotolewa kama viambatanisho vifanane na vile vinavyotangazwa kwenye zabuni ambazo pia zitatangazwa kwa njia ya vitabu (Hard Copies).

MWISHO WA UWASILISHAJI

